# KAPSABET HIGH SCHOOL

**102/2 -KISWAHILI -KARATASI YA 2**

*MOCK 2023*

JINA.......................................................DARASA...........................................

NAMBARI YA USAJILI.........................TAREHE.....................SAHIHI...........

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**KISWAHILI ( LUGHA)**

**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

- Jibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- Karatasi hii ina kurasa kumi. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| **1.** UFAHAMU | **15** | |
| **2.** UFUPISHO | **15** | |
| **3.** MATUMIZI YA LUGHA | **40** | |
| **4.** ISIMUJAMII | **10** | |
| **JUMLA** | **80** | |

KAPSABET MOCK 2023

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Ushauri na uelekezaji ni mojawapo ya mikakati ambayo inatumiwa na taasisi na mashirika mengi katika kurekebisha tabia. Msimamo wa kijadi kuwa adhabu kali ndiyo njia mufti ya kumshinikiza binadamu kuacha mienendo hasi unaendelea kufifia na mahali pake kutwaliwa na nasaha na ushawishi. Hata katika mazingira magumu kama gerezani, ushauri na uelekezaji umeonekana kuzaa matunda kwa kuwasaidia wafungwa kubadili mienendo hasi na kukabiliana na makali ya matendo yao.

Kila mwanajamii, wazee kwa vijana, wake kwa waume, wenye furaha kwa wenye majonzi huhitaji nasaha. Nasaha humwezesha mtu kustahimili hali ngumu katika maisha. Wanaougua magonjwa sugu kama vile iri huhitaji ushauri ili kuishi kwa mitazamo chanya na kupunguza makali ya unyanyapaa na hali ya kujihurumia inayotokana na maradhi hayo.

Halikadhalika, binadamu huhitaji mawaidha wakati anapovuka kutoka daraja moja la maisha hadi jingine. Kila awamu katika maisha ya binadamu huwa na changamoto, majukumu na matarajio yake. Maarusi, kwa mfano, huhitaji nasaha ya kuwawezesha kukabiliana na changamoto za ndoa. Aidha vijana wanaotiwa jandoni hihitaji ushauri wa kuwasaidia kuyamudu majukumu ya utuuzima. Si ajabu kuwa tangu jadi manyakanga wamekuwa wakiwausia wanaotiwa jandoni kuhusu kunga za utuuzima.

Ingawa kila mwanajamii anahitaji ushauri na uelekezaji, vijana ndio wanaouhitaji zaidi kwa sababu hawana uzoefu mpana wa maisha. Vijana wanaohitimu masomo ya shule za upili, kwa mfano, wanahitaji kuelekezwa kuhusu taaluma katika vyuo vikuu, umuhima na mahitaji ya taaluma hizo. Isitoshe, wakati wa kukfanya mitihani vijana huhitaji nasaha.

Mazingira ya binadamu hubadilika, nayo maisha yake hutwaa mabadiliko yanayotokana na hali mpya. Baadhi ya watu wanapojipata katika mazingira mageni wasiyoyaweza, hupatwa na woga au unyonge Fulani ambao huenda ukawaathiri. Wengine, pengine kwa sababu ya maisha duni ya awali, huweza kuathiriwa na kujiona kuwa wenye thamani ya chini wakijilinganisha na wenzao. Kuna wanafunzi au hata wafanyikazi ambao kwa sababu ya kutofikia malengo yao shuleni au kazini, hufa moyo na hata kutaka kuiacha shule au kazi hiyo. Watu kama hawa huhitaji nasaha ili wajikubali jinsi walivyo na hata waweze kutumia udhaifu wao kuboresha maisha yao ya usoni.

Wengi hudhani kuwa wanaohitaji nasaha ni wale wenye matatizo tu. Ukweli ni kwamba, hata wale ambao wanaonekana kuwa na furaha na vyeo wanahitaji ushauri wa aina Fulani. Wenye mali, kwa mfano, wanaweza kushauriwa kuhusu namna ya kuwekeza ili wasifilisike. Viongozi nao wanahitaji nasaha ili waandame sera bora za uongozi pamoja na jinsi ya kuishi kwa mwamana na wanajamii wenzao.

KAPSABET MOCK 2023

Ushauri na uelekezaji, kwa hakika, unahitajika katika nyanja zote za maisha. Ni muhimu kukumbuka kuwa ushauri huanzia nyumbani. Mzazi au mlezi ndiye mshauri wa kwanza. Haifai wazazi kuchelea kuwashauri watoto wao mapema, kwa maana mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.

**Maswali**

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

b) Tofautisha urekebishaji tabia wa kijadi na wa kisasa. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

c) Taja mazingira yoyote manne ambapo binadamu huhitaji nasaha na uelekezaji. (alama 4

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

d) Eleza umuhimu wa kushauri watu wafuatao: (alama 2)

(i) Viongozi.

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(ii) Wenye mali.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

e) Wazazi wasiowausia watoto wao wataathirika vipi hatimaye? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………



KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL

KAPSABET MOCK 2023

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

f) Andika methali yoyote inayohusiana na nasaha. (alama 1)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)

(i) Unyanyapaa.

.............................................................................................................

(ii) Manyakanga

.............................................................................................................

(iii) Mitazamo chanya.

.............................................................................................................

2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:**

Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima tujaribu kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya kugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ikiwa imeandikwa hasa huwa ni aina ya lugha ya mazungumzo vile vile. Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza upatikanao katika shule – kama vile michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa na haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha.

Ujuzi wa kila siku hutasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajapata kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile alivyo. Vile vile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika kusoma. Kwa hivyo kwa njia fulani mambo



KAPSABET MOCK 2023

yote juu ya ujuzi wa kila siku husaidia kufahamu mambo yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amesifiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati ujao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambaye amepatikana na mambo kama hayo hana budi kufahamu vizuri zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabu lakini lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi lakini katika lugha nyingine karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu. Inambidi mwanafunzi anayejifunza asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya shani, na juu ya mahali pageni ili kupata ujuzi wa mambo mengi mbali mbali.

**Maswali**

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65. (alama10,2 za utiririko)

**Nakala chafu**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**Jibu**:

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………



KAPSABET MOCK 2023

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho. (Maneno 30, alama 5, 1 ya utiririko).

**Maandalizi:**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**Jibu:**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

KAPSABET MOCK 2023

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika maneno yenye sifa zifuatazo za sauti:

i) Kilainisho ghuna cha midomo, irabu ya mbele-juu, kipua ghuna cha midomo, kizuiwa ghuna na irabu ya nyuma-wastani. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

ii) Kikwaruzo hafifu cha ufizi, irabu ya chini-kati, kikwamizo cha mdomo-meno hafifu, irabu ya mbele-juu. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

b) Tunga sentensi ukitumia nomino ya ngeli ya **KU** pamoja na kirai husishi cha uhusiano. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

c) Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu katika kitenzi hiki. (alama 3)

Kilivijisha.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

d) Yakinisha kwa **udogo** ukitumia kiambishi cha masharti ya **uwezekano**. (alama 2)

Mtoto aliyeiba kitabu hajakamatwa.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………





KAPSABET MOCK 2023

e) Andika upya sentensi kulingana na maagizo. (alama 1)
Kiroboto huyo alituuma.Kiroboto aliuawa.(Tumia kivumishi kirejeshi cha kati kuunganisha sentensi hizi.)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

f) Eleza Matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mola atakukirimu ukimtolea sadaka.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

g) Andika upya sentensi hii kwa wakati ujao hali katavu. (alama 2)
Mwanariadha alishiriki mbio za Tokyo.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate **mji** na **mchi**. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

i) Unda kitenzi kutokana na nomino **maskani**, kisha ukitungie sentensi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

j)Bainisha kiima na yambwa katika sentensi hii. (alama 2)

Omari alipewa vipuli na fundi stadi kwa bahasha.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

KAPSABET MOCK 2023



KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………..

j) Tunga sentensi katika hali ya wastani ukitumia kihusishi cha hali. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

..............................................................................................................................

k) Ainisha aina za vishazi katika sentensi hii. (alama 2)

Marekebisho ya katiba ya BBI yatapita iwapo wananchi watahusishwa.

…………………………………………………………………………………………

…………………………..………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

l) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha mstari. (alama 2)

Zohali na Zuhura ni majina ya sayari.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

m) Tunga sentensi **moja** ya kuonyesha Matumizi mawili ya vielezi vya silabi moja. (alama2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………..………………………………………………………………

……………………………………………………………...........................................

n) Andika kinyume cha maneno yafuatayo. (alama 2)

Dhahiri……………………………………………………………………………...

..............................................................................................................................

Kavu……………………………………………………………………………………...

..............................................................................................................................

o) Tambua hali katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Ukulima wa sampuli hii wasumbua wengi.



KAPSABET MOCK 2023

…………………………………………………………………………………………

……………………………….………………………………………………………..........

p) Eleza maana ya msemo **shika sikio**. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

q) Tumia kibadala cha kiasi cha kuonyesha nafasi katika orodha kwenye sentensi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

r) Andika kwa wingi sentensi hii. (alama 2)
Ukwato wa mnyama huyo aliufikisha ufuoni.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

s) i) Tunasema baraza la wazee**……………………**wa wagomaji na **……….…………**la nafaka. (alama 2)

ii) Audhubilahi ni tunapoapa**……………………**.tunapokana na …………………………... tunapohimiza. (alama 2)

4. **<u>ISIMU JAMII ( ALAMA 10)</u>**

**Mtu 1:** Je, familia ya mahabusu huyo imetoa bond?

**Mtu 2 :** Idont think so. Na wakiendelea kuchelewa huyo atapandishwa...

a ) Tambua sajili ya kifungu hiki. ( alama 2)

..........................................................................................................................

b) Bainisha sifa nane za sajili hii. ( alama 8)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

KAPSABET MOCK 2023

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

KAPSABET MOCK 2023